A&S6 - Wajulishe walaun jinsi wote, wape [illegible] AS RAS 3/1/19

36

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013
Barua pepe: ps@pmoralg.go.tz

Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
Jengo la Mkapa,
Barabara ya Mlezi
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. CCB 215/443/01

03.01.019

02/01/2019

Makatibu Tawala wa Mikoa,
**TANZANIA BARA**

## YAH: UFAFANUZI JUU YA VIWANGO VYA POSHO ZA WAHESHIMIWA MADIWANI

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

OR-TAMISEMI imepokea Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Mapendekezo ya taarifa ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) juu kuwepo kwa tofauti katika stahili za malipo ya vikao na posho za kujikimu kwa Waheshimiwa Madiwani kwa baadhi ya Halmashuri.

Ili kuondoa tofauti za ulipaji wa Posho za Madiwani baina ya Halmashuri moja na nyingine, waelekezeni Wakurugenzi wa Halmashuari katika Mikoa yenu kuwa;

i. Posho za Waheshimiwa Madiwani za kuhudhuria vikao zinapaswa kulipwa kwa kiwango ambacho kimeainishwa katika waraka Kumb. Namba CHB/443/ 01 wa tarehe 26/11/2007 na kusisitizwa katika waraka Kumb. Na PM/P/1/567/59 wa terehe 16/08/2012 ambapo ni shilingi 40,000.

ii. Posho za Madiwani kwa mwezi zinapaswa kulipwa kwa kuzingatia Waraka Kumb. Na. CCB.215/443/01/50 wa tarehe 23/12/2014 kwa kiwango cha 350,000 na Posho za mwezi za Mameya na Wenyeviti wa Halmashuri zinapaswa kulipwa kwa kuzingatia waraka Kumb Na. CCB.215/443/01/60 wa tarehe 10/04/2015 kwa kiasi cha Shilingi 400,000



Scanned by CamScanner

Posho za Madaraka kwa mwezi zinapaswa kulipwa kwa Waraka Kumb. Na. PM/P/1/567/59 wa tarehe 16/08/2012 kama ifuatavyo.

a) Wenyeviti wa Kamati wanalipwa kiasi cha shilingi 80,000.
b) Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Miji wanapaswa kulipwa kiasi cha shilingi 250,000 hadi 300,000
c) Meya wa Halmashuri za Manispaa wanapaswa kulipwa 300,000 hadi 350,000
d) Meya wa Halmashauri za Majiji wanapaswa kulipwa 400,000 hadi 450,000.

Posho za kujikimu kwa Waheshimiwa Madiwani inapaswa kulipwa kwa kuzingatia mahali/sehemu na umbali Diwani anapotoka. Msingi mkubwa wa kuzingatiwa ni kuwa Diwani husika sharti awe amesafiri na kulala nje ya makazi yake ili aweze kuhudhuria kikao siku inayofuata. Posho hizo hutumika kulipia gharama za malazi/hoteli na zinalipwa kulingana na hadhi ya mji husika (Kijiji, Kata, Wilaya,Mji,Manispaa au Jiji). Hivyo, Madiwani ambao hawatoki mbali na wala hawalazimiki kulala nje ya makazi yao hawastahili kulipwa posho za kujikimu.

Waheshimiwa Madiwani ni Viongozi wa Halmashauri hivyo wanastahili kulipwa kiwango cha posho za kujikimu sawa na Viongozi wengine wa Halmashauri kama vile Wakurugenzi na Wakuu wa Idara. Viwango vya Posho za kujikimu vinapatikana katika Waraka Kumb. Na. CAC/17/45/01/100 wa tarehe 24/11/2014 uliotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi.

Nashukuru kwa ushirikiano.

Dkt. Zainab A. S. Chaula
KAIMU KATIBU MKUU

akala: Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya

Scanned by CamScanner